# HALMASHAURI YA MJI GEITA

Shule ya Sekondari Nyankumbu,
S.L.P 140,
**GEITA**

Kumb.Na.NGSS/J I/1 22/12/2022

Jina la Mwanafunzi: ................................... SIMU: 0754650940/0735650940

..................................

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI NYANKUMBU WILAYA YA GEITA MKOA WA GEITA, MWAKA 2023**

## 1.0 UTANGULIZI

1.1 Ninayo furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari ya Wasichana NYANKUMBU katika Kidato cha kwanza 2023.

Kwa niaba ya Bodi ya shule,Walimu, Wafanyakazi na wanafunzi wa shule hii, nakupongeza na kukukaribisha kwa moyo wa dhati na kindugu.

Shule hii ipo Umbali wa **Kilomita 6** Kusini mwa Halmashauri ya **Mji GEITA.Usafiri wa Mabasi kutoka Stendi Kuu hadi Kituo cha Mabasi NYANKUMBU unapatikana, Nauli ni Sh.500/= au Sh.2,000/= kwa PIKIPIKI.**

1.2. Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 9/1/2023 Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe hiyo hadi tarehe 16/1/2023 ndani ya siku saba.Hata hivyo kutakuwepo na **Kikao cha Wazazi wa Kidato cha Kwanza Tarehe 6/1/2023 saa 4.00 asubuhi** kwa ajili ya ufafanuzi wa utoaji wa Elimu ya Sekondari. Kila mmoja lazima ahudhurie Kikao hicho nyeti.

1.3 Ukiwa hapa shuleni utakuwa na wajibu wa kusoma kwa bidii zote, kufuata Kanuni,Taratibu na Sheria za Shule na kushiriki katika Mipango ya Elimu ya kujitegemea. Shughuli zozote utakazozifanya shuleni hapa zinatahiniwa kila siku na ni sehemu ya Mtihani wa Kidato cha Nne.

1.4 Kuchaguliwa kwako kujiunga na Elimu ya Sekondari ni **BAHATI** na wala si stahili yako, Hivyo una **DENI** Kubwa kwa Nchi yako, Serikali yako na ni kama umetumwa na wananchi walio Vijijini/ Kijijini kwako ulikotoka. Hivyo wanakutegemea uvune chochote Shuleni na hatimaye urudi kuwasaidia ukishavuna ulichopanda.

1.5 (a) Shule hii ni MAALUMU kwa wanafunzi wa KIKE tu, wanafunzi wanasoma kwa bidii kwa malengo ya kupata ufaulu wa **DIVISHENI 1** . Ni jukumu lako Mzazi kuhakikisha kuwa mwanao anapata mahitaji yake ya lazima ili apate muda mrefu wa kujisomea kwani Elimu ya Sekondari inahitaji mwanafunzi ajitafutie maarifa zaidi, akiongezea kwa kile anachopatiwa na mwalimu.

(b) Ikumbukwe kuwa jukumu la kuwalea wanafunzi ni letu sote; Wazazi na walimu, kwa hiyo unapohitajika hapa shuleni lazima ufike kuangalia tabia, maendeleo ya mwanao kitaaluma na mwenendo wake. Kushindwa kuitikia wito wa shule kunaweza kusababisha mwanao kusimamishwa masomo na hata wewe kuchukuliwa hatua za kisheria.

(c) Uhamisho usio wa lazima au holela kwa wanafunzi wa shule hii hautakubaliwa. Uhamisho utakaotolewa ni ule wa lazima na halali wenye viambatanisho vya sababu za kuomba uhamisho huo; nao utatolewa mara mbili kwa mwaka yaani mwezi Juni na Desemba.

Hivyo utaijulisha shule mapema ili taratibu za uhamisho zifanyike kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia.

(d) Ni kosa **kisheria** kwa mzazi /mlezi kumuozesha mwanae akiwa bado ni mwanafunzi. Mwanao lazima amalize shule. Ni haki yake ya msingi na ya kikatiba wewe mzazi kumsomesha na Kumgharamia mahitaji yote ya shule pamoja na CHAKULA na MATIBABU.

(e) Ili tuweze kupashana habari juu ya maendeleo ya mwanao, itakubidi kujulisha shule Anuani/ Namba ya SIMU yako Kamili, hii ni pamoja na unapobadilisha Anuani/Namba ya SIMU.

(f) Mwanao akishajiunga na shule hii atalazimika kushiriki shughuli zote za shule bila kujali matakwa ya Mzazi/Mlezi wake. .

(g) Wakati mwanao akiwa mwanafunzi wa shule hii atashiriki na kuhudhuria michezo shuleni na hivyo awe na nguo za michezo kwa ajili ya mazoezi.

(h) Mwanao atalazimika kuhudhuria siku zote **194** za masomo, kama itatokea shida yoyote ya lazima kutofika shuleni, utatoa taarifa ya maandishi.. Pengine unaweza kufika mwenyewe kumuombea ruhusa.

(i) Sababu kubwa ya mwanao kuwepo shuleni ni kusoma kwa bidii na kufaulu Mitihani yote ya **Ndani** na **Nje** ya shule kwa **Kiwango cha Wastani wa A au B**. Mzazi/Mlezi hakikisha mwanao anahudhuria masomo yote na kuyafaulu kwa Gredi A au B. Lugha ya mawasiliano shuleni ni Kiingereza au Kiswahili inapobidi. Akishindwa kufikia Wastani wa shule/Division I au II atarudishwa kwenye *CATCHMENT AREA* yake (Eneo anakotoka).

(j) Katika jamii yoyote ile wakosaji huchukuliwa hatua mbalimbali za kinidhamu. Hapa shuleni adhabu hutolewa kwa wakosaji wa nidhamu vilevile. Hivyo Mzazi/Mlezi hataruhusiwa kuingilia hatua za kinidhamu zinazochukuliwa dhidi ya wakosaji. Kufanya hivyo kunaweza kusababisha mwanao kupoteza nafasi hii aliyopewa. Hali kadhalika kama mwanao atakataa adhabu yoyote aliyopewa anaweza kupoteza nafasi yake kwa mujibu wa sheria za shule.

(k) Ni jukumu lako Mzazi kuhakikisha kuwa mwanao anaishi maisha ya uanafunzi anapokua nje ya shule yaani nyumbani. Shule haitasita kumchukulia hatua za kinidhamu dhidi ya utovu wa nidhamu nje ya shule. Anatakiwa kubaki ni mwanafunzi wakati wowote awe shuleni au nje ya shule.

## 2.0 MAHITAJI MUHIMU.

### 2.1 **SARE YA SHULE:**

- Mashati 2 meupe ya mikono mifupi yasiyobana na hayana urembo wowote (TOMATO)
- Sketi 2 Ndefu za Rangi ya **BLUU BAHARI (Kitambaa cha SURUARI)** na zisizobana zenye marinda yasiozidi 8 (**Marinda ni matatu matatu yanayotazamana kushoto na kulia**), mkanda wa sketi ni INCHI 2 na Urefu ni INCH 8 kutoka kwenye magoti au siketi ndefu.Iwapo utakosa kitambaa sahihi kitapatikana shuleni.

Waislam wanaruhusiwa kuvaa Mashati ya mikono mirefu na mtandio mweupe.

- Tai 2 zinazofanana na Rangi ya Sketi.
- VIATU VYA NGOZI VYEUSI (Kisigino BUTU) na sio BOOT
- Soksi jozi 2 au zaidi STOCKING NYEUPE.
- SWETA Rangi ya BLUU BAHARI. Kwa kuwa zinashonwa Kiwandani utaipata shuleni.
- T-shirt rangi ya dark blue yenye kola ya kaki na MHURI utaipata shuleni
- Track-Suit rangi ya DARK BLUE yenye michirizi myeupe
- Nguo za Michezo (Track Suit/JEZI rangi ya njano na Raba.)
- GAUNI la kushindia la heshima kitambaa cha kunguru(TETRON ya DRAFT) Damu ya mzee (Maruni)

- Godoro ft 21/2 x 6, CHANDARUA FT 31/2 X 6 na MASHUKA 2 rangi ya Bluu,mto 1 na FOLONYA 2 rangi ya BLUU. Magodoro ya SUPER BANCO unaweza kulipata shuleni kwa Sh.55,000/=
- BLANKETI 1 NYEPESI, Doti ya kitenge au khanga na Taulo kwa ajili ya kuongea
- Sahani , Kikombe,Bakuli, Kijiko na KIDUMU cha Maji ya kunywa na Ndoo ya kuogea
- Kandambili za kuongea na Viatu (Open shoes) za kushindia

NB: - Unaweza kupata SWETA kwa urahisi rangi husika kwa MASISTA  GEITA SIMU NA. **0788 527 064** na T- SHIRT zenye NEMBO ya shule yetu **SIMU Na.0756 544 001**

- **NGUO ZA NYUMBANI haziruhusiwi shuleni**

2.2 Daftari kubwa 12(Counter Books), Kamusi ya KIINGEREZA, kalamu, Mkebe wa hesabu na begi la kubebea madaftari (**School bag**), na faili moja

2.3 Chakula, nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani na Matibabu pamoja na fedha ya kujikimu

2.4 Nauli ya wanafunzi wa Bweni/Hostel kwenda shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo

2.5 Mfagio chelewa/ Mfagio brash kwa ajili ya usafi.

2.6 **GHARAMA ZA UENDESHAJI WA HOSTEL KWA MWAKA**

Katika Mwongozo wa Serikali wa Elimu Bila Malipo - 2016, Wazazi/Walezi wana jukumu la kuchangia CHAKULA na MATIBABU kwa watoto wao shuleni.Hivyo mzazi/mlezi anayeridhia kumleta mwanae Hostel atatakiwa kuchangia CHAKULA cha mwanae kwa **mwaka SH.660,000/=**.Kiasi hiki ni sawa na **Sh. 2,000/= kwa siku kwa MILO 3** yaani UJI wenye SUKARI, Chakula cha MCHANA na USIKU. Mzazi/Mlezi unaweza kuchangia AWAMU 1 au 2 au ili mradi mtoto asikose Chakula shuleni**.**

**FEDHA hii ilipwe kwenye AKAUNTI YA SHULE  NYANKUMBU S.S SELF- RELIANCE A/C NA. 31003300026 NMB** na kuwasilisha **SLIP ya MALIPO hayo shuleni.**

## 2.7 IWAPO UMEKUBALI UCHAGUZI HUO WA KUJA SHULE HII BASI UFANYE YAFUATAYO:

(i) Kujaza FOMU NA. NGSS/S.1942/1 ya kukubali na kuirudisha haraka iwezekanavyo shuleni

(ii) Naambatanisha FOMU ya Hospitali Kumb. Na. NGSS/S.1942/2. Inakupasa uende kupimwa na Bwana Mganga wa Serikali. Ufikapo shuleni lazima ulete **FOMU** hiyo ikiwa na uthibitisho wa Mganga wa Serikali ikionyesha hali ya Afya yako.

(iii) DARASA lako utapangiwa baada ya kuripoti shuleni

(iv) Shule hii itafunguliwa tarehe .. Siku kwa wanafunzi wote. Fika shuleni ukiwa na Mzazi/Mlezi wako saa 4.00 asubuhi. Kutakuwa na Kikao cha Wazazi kwa ufafanuzi zaidi.

(v) **MUHIMU SANA**: Utaleta **CHETI CHA KUZALIWA** kitakachothibitisha **URAIA** wa Nchi ulikozaliwa. Nakala yake itatunzwa kwenye FAILI lako shuleni.

## 3.0 SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na.10 ya mwaka 1985.Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais-

TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

## 3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE AU KUSIMAMISHWA MASOMO.

(a) Kashfa yoyote kwa Taifa na Viongozi wa Taifa.
(b) Wizi na kuharibu mali ya UMMA kwa makusudi.
(c) Kuolewa ukiwa bado mwanafunzi ni pamoja na kuwa na mimba
(d) Kutohudhuria shuleni kwa muda mrefu bila taarifa au sababu za msingi zilizothibitishwa.
(e) Kutenda kosa likakalothibitishwa na POLISI uwe umefikishwa Mahakamani au la.
(f) Kukataa adhabu shuleni kwa makusudi.
(g) Kupiga au kupigana
(h) Ulevi wa aina yoyote ile na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine,mirungi, kubeli n.k
(i) Kugoma au kushawishi mgomo unaoweza kusababisha vurugu shuleni au kwenye jamii.
(j) Kutembelea au kukutwa ndani ya majumba ya starehe,vilabu vya pombe na majumba ya kufikia wageni (**GUEST HOUSE**)
(k) Kudharau BENDERA YA TAIFA
(l) Kuwa na **Simu ya mkononi shuleni**

## 4.2 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na:-

(i) Mapambo yoyote kwenye mwili wake, heleni na vipuri ukiwa na sare ya shule
(ii) Kanda mbili au viatu vya matairi ya gari haviruhusiwi shuleni
(iii) Makucha marefu pamoja na kupaka rangi au hina kwenye kucha
(iv) Nywele ndefu ila unaruhusiwa kusuka msuko wa ROZA/Twende kilioni
(v) NGUO FUPI na zile zinazoubana mwili ni marufuku shuleni
( vi) Tabia ya kutoheshimu Viongozi , Wazazi,Walimu, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.

Ili ufaulu vizuri lazima utekeleze yafuatayo:

(vii) Mahudhurio mazuri katika kila SOMO na shughuli ndani na nje ya shule kulingana na Ratiba ya shule.
(viii) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni ( Preparation) na kusoma masomo yote.
(ix) Kuwahi katika kila shughuli za shule na kuzingatia **Ratiba ya shule** wakati wote
(x) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa, kutunza usafi wa mwili, mavazi na Mazingira ya shule.Unadhifu ni lazima wakati wote.

**Tafadhali soma kwa makini Maelezo/Maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA NYANKUMBU**

**HIGH PERFORMANCE IS OUR STANDARD**

**G K MUGASHE**

**MKUU WA SHULE**

**HALMASHAURI YA MJI GEITA**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA NYANKUMBU**

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

**NGSS/E.10/1**

1. Jina la mwanafunzi: …………………………………………………………………………….........................
2. Tarehe ya kuzaliwa: . ………………………
3. Kijiji/Mtaa ulipozaliwa:……………………… Wilaya ……………………….. ………………………
4. Dini ……………..……………………… Dhehebu ……..………………………………
5. Ni raia wa Tanzania? NDIYO/ HAPANA. Ni raia wa …………………………………….
6. Darasa ulilomaliza: ……………………………………………………………………………….
7. Shule uliyoanzia kusoma Darasa la Kwanza;………………………………………..
8. Mwaka ulioanza Darasa la Kwanza; ………………………………………………………
9. Shule uliomalizia Darasa la saba;…………………………………………….
10. Jina kamili la Mzazi/Mlezi ……………………………………………Na. ya SIMU………………………
11. Anuani kamili ya Mzazi/ Mlezi ………………………………………………………………………………………………..
12. Mahali anapoishi Mzazi/Mlezi ………………………………………………………………………………………………
13. Umbali kutoka unapoishi hadi shuleni ……………………………………………………………………………….
14. Mzazi/Mlezi wako anafanya kazi gani? …………………………………………………………………………..
15. Taja jina kamili la Balozi wako …………………………………………………………………………………………….
16. Taja jina la Mtendaji wako wa kijiji chako………………………………………………………………
17. Taja jina la Mtendaji wa kata yako ……………………………………………………………………………….
18. Unapendelea kucheza Michezo gani? ……………………………………………
19. (Weka tiki sehemu ulipo) Nina wazazi wote ………………..Sina wazazi……………

    Nina mzazi mmoja ……………… Baba/Mama.
20. Je uko tayari kuendelea na Elimu ya Sekondari………………………………………….........

**HALMASHAURI YA MJI GEITA**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA NYANKUMBU**

**FOMU YA KUKUBALI NA MKATABA**

**NGSS/S.1942/2**

Mimi mwanafunzi ………………………………………… Nimesoma na kuyaelewa maelezo yote ya kujiunga na Elimu ya Sekondari katika Shule ya Sekondari ya Wasichana NYANKUMBU iliyoko katika Wilaya ya GEITA , Halmashauri ya Mji GEITA.

NAKUBALI kujiunga na Elimu ya Sekondari.Naahidi kumaliza shule kwa kutumia vizuri nafasi niliyopewa iwapo nitaipoteza nafasi hii hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yangu. Pia naahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na Makosa ya Jinai

**SAHIHI**; ……………..

Mimi Mzazi /Mlezi ……………………………………….….. Nimesoma na kuyaelewa maelezo ya Fomu ya kujiunga na Elimu ya Sekondari kwa mwanangu ………………………….………, Naahidi kumsomesha na kumpatia **Mahitaji** yote ya shule kama Serikali yetu inavyoelekeza. Iwapo nitakiuka taratibu niwajibishwe kwa mujibu wa Sheria.

**SAHIHI**: ……………………

**SAHIHI NA MUHURI WA MTENDAJI WA KATA……………………., TAREHE……………..**

*"FOMU hizi zijazwe na kurejeshwa shuleni"*